

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA**  
**HUDUMA YA AFYA YA UZAZI NA MTOTO**

**Utangulizi**

Wilaya ya ngara ina jumla ya vituo 61 vinavyotoa huduma ya afya ambapo hospitali zipo 3 (1 ya serikali) vituo vya afya vitano na zahanati 53. Kati ya hivyo vituo 54 (88.5%) vinatoa huduma ya afya ya uzazi na mtoto na vituo 4 (6.5%) vinatoa huduma ya uchunguzi wa awali wa saratani ya shingo ya kizazi.

**WALENGWA WA AFYA YA UZAZI NA MTOTO KATIKA WILAYA YA NGARA**

Wilaya ya Ngara inajumla ya watu 388,289, walengwa katika uzazi wa mpango ni 89,966, walengwa wa wajawazito ni 18,559 na walengwa katika chanjo ni 18,559

**MAENDELEO YA AFYA YA UZAZI NA MTOTO 2016 - JUNE 2018**

ANC	Viashiria	2016	2017	Jan-June 2018	Lengo
	Waliohudhuria kliniki chini ya wiki < 12 weeks	11.50%	32.30%	53.30%	80.00%
	wajawazito waliohudhuria mahudhurio manne	35.10%	46.30%	62.40%	80.00%
	wajawazito waliopata SP ya pili	69.50%	69.50%	80.10%	80.00%
	wajawazito waliopata nyongeza ya vidonge vya damu	79.50%	55.30%	89%	80.00%
PNC	Asilimia ya wakinamama waliohudhuria baada ya kujifungua ndani ya saa 48	52.80%	68.40%	36.90%	80.00%
	kiwango cha wakinamama na watoto waliofanyiwa uchunguzi ndani ya siku 3-7	27.10%	39.80%	59.50%	80.00%
Wodi ya Uzazi	Kiwango cha kujifungua kwa kinamama katika vituo vya kutolea huduma	66%	78.40%	89%	90.00%
	kiwango cha kinamama waliozalishwa na watoa huduma wenye ujuzi	93%	93.50%	93.30%	90.00%
UZAZI WA MPANGO	kiwango cha wateja waliojiunga njia za kisasa za uzazi wa mpango	32.70%	32.30%	40.40%	45.00%
Chanjo	Kiwango cha watoto waliopata chanjo ya DPT/Penta dozi ya tatu	88.30%	88.40%	80.90%	90.00%

## VIFUATAVYO NI VIFO VITOKANAVYO NA UZAZI

	Octoba - Desemba- 2017	JAN-March 2018	April – Juni 2018
WATOTO WALIOFARIK NDANI YA SIKU SABA BAADA YA KUZAZLIWA.	7	6	3
WALIOZALIWA WAFU (FSB)	3	9	5
WALIOZALIWA WAFU (MSB)	3	4	3
JUMLA	13	19	11

## VIFO VYA WAZAZI KWA KUENZIA MWAKA 2017 MPAKA JUNE 2018

VISABABISHI	JAN- Juni 18	%
KUTOKA DAMU NYINGI (PPH)	2	18.18
UAMBUKIZI	3	27.7
UZAZI PINGAMIZI (OBSTRUCTED LABOUR)	1	9.0
UPUNGUFU MKUBWA WA DAMU (ANAEMIA)	2	18.18
MAGONJWA YA MOYO (HEART DISEASE)	1	9.0
SABABU NYINGINEZO (DIC)	2	18.18

## **MAFANIKIO**

- ✓ Ongezeko la kiwango cha kina mamawa jawazito wanaoanza hudhuria la kwanza la kliniki wakiwa chini ya umri wa wiki 12 toka 32.3 (2017) hadi 53.3% (June 2018)
- ✓ Ongezeko la kiwango cha kinamama waliohudhuria mahudhuria manne katika kliniki ya wajawazito toka 46.3% (2017) hadi 62.4% (June 2018)
- ✓ Ongezeko la kina mama waliopatiwa dawa za SP ya dozi ya 2 kwa ajili ya kukinga Malaria kwa wajawazito toka 69.5% (2017) hadi 80.1% (June 2018)
- ✓ Ongezeko la kiwango cha wajawazito waliopatiwa dawa za madini chuma “folic acid/FEFO”
- ✓ Ongezeko la kina mama na watoto wanaorudi kwa ajili ya uchunguzi baada ya kujifungua ndani ya siku tatu hadi saba.
- ✓ Ongezeko la kiwango cha wajawazito wanaojifungulia vituo vya huduma za afya toka 78.4% (2017) hadi 89% (June 2018)
- ✓ Ongezeko la kiwango cha wazazi waliozalishwa na watoa huduma wenye ujuzi.
- ✓ Ongezeko la wateja waliojiunga na njia za kisasa za uzazi wa mpango toka 32.3% (2017) hadi 40.4% (2018).
- ✓ Ongezeko la wateja wanaokuja kwa ajili ya uchunguzi wa awali wa saratani ya shingo ya kizazi
- ✓ Upatikanaji wa dawa muhimu za wazazi vituoni mfano Mebendazo, Folic Acid, na SP.

## **CHANGAMOTO ZILIZOPO**

- Uchache wa watumishi kwenye vituo vya huduma za afya.
- Ukosefu wa vipimo muhimu vituoni kama kipimo cha wingi wa damu kwa ajili ya wajawazito na watoto umri chini ya miaka mitano.
- Kuwa na vituo vichache vinavyotoa huduma ya dharula ya kujifungua (CEMOnc sites)
- Vituo vichache vinavyofanya uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi.
- Watumishi kutopata mafunzo rejea mara kwa mara ili kuendana na wakati.
- Akina baba kutojijhusisha sana na huduma za uzazi wa mpango.

## **NAMNA YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO**

- Wizara itoe kipaumbele kwa wilaya ya Ngara ikizingatiwa ni wialaya ya pembezoni mwa nchi kutuma watumishi wa kutosha angalau kila kituo kiwe na watumishi watatu.
- MSD iwe na uwezo wa kuwa na vipimo muhimu kwa ajili ya vituo kuweza kufanya manunuzi na kurahisisha upatikanaji wake.
- Tunaomba na vituo vya afya Bukiriro na Lukole viwekwe kwenye mpango wa kuboreshwa ili viweze kupunguza umbali wa rufaa kwenye maeneo hayo na kusaidia kupunguza vifo vya wazazi na watoto wachanga.
- Wilaya inajiandaa kuongeza vituo vinavyotoa huduma ya uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi ili kurahisha huduma kwa akina mama.

- Wilaya kwa kuwatumia wadau mbalimbali imekuwa ikiwapeleka watumishi kupata mafunzo rejea pia kupitia usimamizi elekezi kwenye vituo vya huduma za afya.
- Hamasa inaendelea kutolewa kupitia mikutano na vyombo vya habari katika kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu na faida za uzazi wa mpango.